**Mwongozo wa Zuio la Matumizi ya Rasilimali na Uhamishaji Watu Usio wa Hiari Kongani ya Kilombero na Unguja.**

**Utangulizi**

FOLUR ni Mradi unaojihusisha na masuala ya Mifumo ya Chakula, Matumizi Endelevu ya Ardhi na Urejeshaji wa Uoto wa Asili, Mandhari na Misitu. Mradi unafadhiliwa na Mfuko wa Mazingira Duniani (GEF) na kutekelezwa na Wizara ya Maliasili na Utalii, kupitia Idara ya Misitu na Nyuki kwa ushirikiano na WWF. Mradi unatekelezwa kwa kipindi cha miaka mitano (2024/25–2028/29).

Mradi unatekelezwa katika Kongani mbili za Kilombero (Tanzania Bara) na Kaskazini Unguja A na B (Zanzibar) kwa kusimamiwa na Ofisi kuu ya Mradi iliyopo Dodoma, Jengo la Wizara ya Maliasili na Utalii, mji wa Serikali Mtumba. Pia mradi una ofisi za Konga; Kongani ya Kilombero ofisi zipo Halmashauri ya Mlimba na Kongani ya Zanzibar ofisi zipo jingo la Idara ya Misitu, mtaa wa Maruhubi.

Lengo kuu la mradi ni kukuza mbinu jumuishi zinazochanganya uzalishaji endelevu wa chakula kwa kuimarisha minyororo ya thamani isiyochochea uharibifu wa misitu hususan zao la mpunga, pamoja na mipango ya utunzani na urejeshaji wa mandhari, ili kulinda na kuendeleza mifumo ya ikolojia. Katika kipindi cha utekelezaji, mradi wa FOLUR unatarajiwa kuchangia katika kuboresha uzalishaji wa mpunga, kulinda rasilimali za asili, na kuimarisha ustawi wa jamii kwa njia endelevu na jumuishi.

**Mpango wa Usimamizi na Usalama wa Jamii na Mazingira – Katazo la Matumizi na Uhamisho Usio wa Hiari.**
Mpango huu wa Usimamizi wa Mazingira na Jamii (ESMP) kuhusu Vizuizi/Katazo la Matumizi ya Rasilimali na Uhamishaji Usio wa Hiari wa Watu (Involuntary Resettlement) unalenga kudhibiti au kupunguza athari za kimazingira na kijamii zitokanazo na utekelezaji wa shughuli za mradi kwa kuweka hatua mahsusi za kupunguza na kudhibiti athari hizo ili kwenda sawa na matakwa ya Mwongozo wa Sera na Taratibu Jumuishi za Ulinzi wa Kijamii za WWF. Mwongozo huu unalenga kuzibaini athari kabla hazijajitokeza, kuziepuka athari hizo au kupunguza madhara ya athari hasi zinazoweza kuathiri wanajamii au mazingira husika.

U**hamishaji usio wa hiari wa watu (Involuntary Resettlement)**
Mradi utaepuka shughuli zozote zitakazohitaji kuhamisha makazi ya watu bila hiari. Ikiwa uhamishaji ni lazima na unatokana na mpango wa matumizi endelevu ya aridhi na maji uliofanywa na kijiji, basi mradi utahakikisha waathirika wanapata stahiki zao kwa mujibu wa shria ikiwa ni pamoja na kufanyiwa uthamanishaji (valuation) na kulipwa fidia sahihi kwa kufuata miongozo na taratibu za nchi na mradi.

**Athari zinazoweza Kujitokeza Wakati wa Utekelezaji wa Shughuli za Mradi**

i. **Athari Chanya Zinazotarajiwa Zitokanazo na Vizuizi vya Matumizi wa Maeneo ya HCV**

| Faida Tarajiwa / Athari Chanya | Maelezo |
|---|---|

| | |
|---|---|
| **i. Urejeshwaji wa uoto wa asili kwa njia za asili (Natural Vegetation Recovery)** | Kudhibitiwa kwa shughuli za kibinadamu kwenye maeneo ya uhifadhi husaidia urejeshwaji wa asili wa uoto kwa kuruhusu miche, miti ya asili, vichaka na uoto wa ardhini kuota na kustawi bila kulazimika kuingilia zoezi hilo. |
| **ii. Uhifadhi wa udongo (Soil Conservation)** | Uoto endelevu utasaidia kupunguza mmomonyoko wa udongo unaosababishwa na upepo na mvua, kuimarisha uthabiti wa udongo na kuboresha rutuba kupitia ongezeko la mabaki ya viumbe hai na mboji asilia. Hatua hizi zitasaidia kurejesha afya ya udongo kwa muda mrefu. |
| **iii. Uhifadhi wa maji (Water Conservation)** | Kuimarika kwa misitu kutaboresha upenyezaji wa maji ardhini, kupunguza mtiririko wa juu ya ardhi na kuongeza ujazaji wa maji chini ya ardhi, hivyo kuboresha udhibiti wa rasilimali za maji. Kwa **LCU ya Zanzibar**, misitu itaendelea kutekeleza jukumu lake kama chanzo muhimu cha maji (*water tower*), wakati kwa **Kilombero**, hatua hizi zitachangia kuongeza mtiririko wa maji kuelekea bwawa la Julius Nyerere Hydropower Project. |
| **iv. Huduma za tabianchi na mazingira (Climate and Environmental Services)** | Urejeshwaji wa misitu utaongeza ufyonzaji na uhifadhi wa kaboni, hivyo kuchangia kupunguza athari za mabadiliko ya tabianchi. Pia, ongezeko la mwavuli wa miti litasaidia kupunguza joto la uso wa ardhi, kuongeza unyevunyevu. |
| **v. Urejeshwaji wa gharama nafuu (Cost-effective Restoration)** | Urejeshwaji wa asili wa mifumo ikolojia unahitaji rasilimali chache ukilinganisha na upandaji miti wa moja kwa moja, hivyo kuwa njia endelevu na yenye ufanisi wa gharama katika kurejesha mazingira yaliyoharibika. |
| **vi. Kuzuia uharibifu wa ardhi (Land Degradation Reversal)** | Ulinzi wa maeneo husika utasaidia kusitisha uharibifu wa ardhi na kurejesha utendaji wa mifumo ikolojia kwa muda mrefu, ikiwemo kupunguza hatari ya kuenea kwa hali za kugeuka jangwa. |
| **vii. Kuimarika kwa bioanuai (Enhanced Biodiversity)** | Kuongezeka kwa uoto kutaboresha makazi ya viumbe kwa kulinda maeneo ya malisho, kuzaliana na makazi ya viumbe mbalimbali, hivyo kuongeza bioanuai katika maeneo ya mradi. |
| **viii. Fursa za elimu na utafiti (Educational and** | Maeneo ya uhifadhi yenye ulinzi yanaweza kutumika kama maabara hai kwa tafiti za ikolojia, ufuatiliaji wa |

| | |
|---|---|
| **Research Opportunities)** | urejeshwaji wa mazingira na elimu ya mazingira kwa jamii na taasisi za utafiti |

ii. **Athari Hasi kutokana na Zuio la Matumizi na Hatua za Kudhibiti/Kupunguza Athari hizo**:

| Wadau/Watu Wanaoathirika | Aina ya Kizuizi cha Upatikanaji | Athari Zinazoweza Kutokea | Hatua za Kupunguza Athari |
|---|---|---|---|
| Wakusanyaji wa kuni na mazao ya misitu | Kuzuiwa kuingia katika maeneo ya misitu/HCV | Kupotea kwa kipato na rasilimali za kaya | Miradi mbadala ya kipato, matumizi endelevu yaliyodhibitiwa, fidia pale inapostahili |
| Wafugaji | Vizuizi vya malisho au njia za mifugo au sehemu za kunyweshea mifugo | Kupungua kwa afya na uzalishaji wa mifugo | Kutenga malisho mbadala, usimamizi endelevu wa malisho na sehemu za kunyweshea maji |
| Wafugaji nyuki na wakusanyaji wa asali | Kuzuiwa kufikia maeneo ya uzalishaji | Kupotea kwa kipato | Ufugaji nyuki wa kisasa nje ya maeneo yenye vikwazo/vizuizi |
| Wakusanyaji wa dawa asilia na mazao ya asili | Vikwazo vya ukusanyaji wa rasilimali | Kupungua kwa upatikanaji wa mahitaji ya kijamii na kiuchumi | Makubaliano ya matumizi endelevu; usimamizi shirikishi |
| Jamii zenye maeneo ya kiutamaduni/kiroho ndani ya misitu | Kuzuia ufikivu wa maeneo ya urithi | Kupotea kwa huduma za kiutamaduni na kiroho | Taratibu maalum za ufikivu; ulinzi wa maeneo ya urithi |
| Wafanyabiashara wadogo wa mazao ya misitu | Kupungua kwa bidhaa za biashara | Kupotea kwa kipato | Mafunzo ya biashara mbadala; mikopo midogo |
| Jamii zinazozunguka maeneo ya HCV | Kuzuia ushiriki wa jamii katika usimamizi wa rasilimali | Kupungua kwa uwajibikaji wa jamii kwenye uhifadhi | Ugawaji shirikishi wa mazao ya uhifadhi |

**Uwasilishaji wa Malalamiko**

Iwapo kutakuwa na malalamiko kutoka kwa watu binafsi, kundi au jamii kutokana na baadhi ya shuguli zinazotekelezwa na mradi, muhusika atatakiwa kuwasilisha malalamiko hayo kwa moja ya njia zilizoainishwa hapa chini. Malalamiko husika yatafanyiwa kazi na muhusika atapewa mrejesho kulingana na aina ya lalamiko.

| **Ngazi ya Uwasilishwaji** | **Namna ya Kuwasilisha** |
| --- | --- |
| Jamii | Baada ya Kutolewa elimu ya miongozo ya mradi, kijiji kitapendekeza jina la mtu, au taasisi iliyopo kijijini mfano CBO/Kanisa/Msikiti ambao utaweza kuwa sehemu ya awali ya kuanzisha mchakato wa Malalamiko. Kitakachokusanywa kitawakilishwa kwenye mradi au wizarani ili kuweza kufanyiwa kazi.<br><br>Mwasiliano ya Muhusika<br><br>Jina (Mtu au Taasisi)……………………………………<br><br>Namba ya simu ……………………………………..<br><br>*Mradi utahakikisha kila kilichowasilishwa kimeingizwa kwenye fumu mahususi ili kipate kufanyiwa kazi na mrejeshwo kutolewa.* |
| Kongani/Halmashauri | Ofisi za Kongani zinaweza pia kutumika kama fursa ya kuanzisha mchakato wa kuwakilisha malalaminko. Kitakachopatikana hapa kitawasilishwa kwa Afisa Muhusika Ngazi ya Makao Makuu au Wizarani.<br><br>Mawasiliano.<br><br>Mlimba<br><br>Joseph Mgana, +255787958877 josephmgana@gmail.com<br><br>Zanzibar<br><br>Miza Khamis +255777332223 mizakhamis@gmail.com<br><br>*Mratibu akiisha kupokea nia ya kuwasilisha lalamiko, atawasiliana na afisa anaeyeshughulikia malalamiko ngazi ya Makao Makuu au Wizara ili mchakato wa Kuanzisha lalamiko rasmi uanze.* |

<table>
<tr><td colspan="2">Ikumbukwe, Ili lalamiko lifanyiwe kazi lazima kujazwe fomu mahususi inayotolewa na Afisa Husika Ngazi ya Makao Makuu au Wizarani kulingana na aina ya lalamiko. Ngazi ya Kongani na Kijiji ni kwaajili ya kumsaidia Muhusika kupata mawasiliano ya Afisa Husika Ngazi ya Makao Makuu au Wizara.</td></tr>
<tr><td>Ngazi ya Kitaifa</td><td>Malalamiko yawasilishwe kwenye Ofisi za Makao Makuu ya Mradi kupitia Mratibu wa Masuala ya Jinsia na Mazingira/Afisa anaeshughulika na Malalamiko.<br><br>Revocatus Kadoshi<br><br>(+255765 456 218 revocatusg@gmail.com)<br><br>au<br><br>Mratibu wa Mradi<br><br>(wanjala.mgaywa@maliasili.go.tz/+255755690187)<br><br>Au<br><br>MkurugenziIdara ya Misitu na Nyuki – Wizara ya Maliasili na Utalii (dfob@maliasili.go.tz/+255755578057)</td></tr>
<tr><td>Kimataifa</td><td>Email: SafeguardsComplaint@wwfus.org<br><br>https://secure.ethicspoint.com/domain/media/en/gui/59041/index.html.</td></tr>
</table>